



S.L.P. 114,  
MUGUMU-SERENGETI  
E-Mail: wmaikona@yahoo.com

12 MEI, 2022

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori IKONA inatangaza nafasi ya kazi

## 1. ASKARI WA WANYAMAPORI (GAME SCOUT)

### Sifa za kuajiriwa

1. Awe mkazi wa kijiji mwanachama IKONA (Hususani Kijiji cha Nyichoka)
2. Awe raia wa Tanzania
3. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 35
4. Awe na elimu ya kuanzia darasa la saba na kuendelea
5. Awe na akili timamu
6. Angalau amepata mafunzo ya Pasiansi na awe anafundishika kazini
7. Asiwe ametiwa hatiani kwa kosa lolote na kutumikia kifungo sio chini ya miezi sita.

### Kazi na Majukumu:

1. Kufanya doria ndani ya eneo la uhifadhi la IKONA WMA na kwenye vijiji vyake wanachama
2. Kudhibiti vitendo vya ujangili nje na ndani ya hifadhi
3. Kusimamia shughuli za uwindaji wa kitalii na utalii wa picha
4. Kulinda binadamu na mali zao dhidi ya Wanyamapori wakali na waharibifu
5. Kukusanya na kulinda nyara za Serikali
6. Kufanya usafi na ulinzi wa kambi
7. Kusimamia uingiaji na utokaji wa watu na mali zao kwenye hifadhi
8. Kukusanya na kutunza vielelezo vya ushahidi na kutoa ushahidi Mahakamani
9. Kukusanya takwimu za Wanyamapori, ndege na mimea

10. Kudhibiti wanyamapori waharibifu
11. Kudhibiti moto kwenye hifadhi na
12. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri

STAHIKI: Viwango vya malipo ya mshahara vitazingatia muundo wa Jumuiya.


Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **27 Mei, 2022 saa 10:00 Jioni.**

Barua zote za maombi zitumwe na kupokelewa ofisi KUU –IKONA WMA kwa anuani ifuatayo;

**KATIBU MTENDAJI,  
JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI IKONA,  
S.L.P 114,  
MUGUMU/SERENGETI.**

Au kwa

Barua pepe: wmaikona@yahoo.com

Limetolewa na;  
  
-----  
**YUSUPH MANYANDA**  
**KATIBU MTENDAJI**  
**IKONA WMA**

